

MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA FEBRUARI, 2017 NA MWELEKEO WA MACHI, 2017

Dondoo za Februari 2017

Taarifa hii inatoa muhtasari wa hali ya viashiria vya hali ya hewa na mwenendo wa mvua katika mwezi uliopita na mwelekeo wa viashiria na mvua kwa mwezi Machi 2017 nchini.

- a) Katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria na maeneo machache ya pwani ya Kaskazini mvua zinazoendelea zinatarajiwa kuungana na kuanza kwa msimu wa mvua katika wiki ya kwanza hadi ya pili ya mwezi Machi, 2017 na kusambaa katika maeneo mengine.
- b) Vipindi vya mvua kubwa vinaweza kujitokeza katika baadhi ya maeneo ya nchi katika kipindi hiki.

1. MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2017

1. 1 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2017

Katika kipindi hiki, maeneo mengi ya Kusini mwa nchi yalipata mvua nyingi zikiwemo mvua kubwa, wakati maeneo ya Kati yalipata mvua kadhaa. Hata hivyo, kuelekea mwishoni mwa kipindi hiki, hali ya vuguvugu katika Bahari ya Hindi pamoja ukanda wa mvua wa ITCZ kusogea kuelekea Kaskazini katika baadhi ya nyakati, kulisababisha mvua za kutosha katika maeneo ya Kaskazini mwa nchi. Pia, vipindi vya upepo mkali vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya Kati na yale ya Kaskazini-mashariki mwa nchi.

2.0 MATAZAMIO KWA MACHI, 2017

2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Maeneo ya kati ya Kitropiki ya Bahari ya Pasifiki yanatarajiwa, kwa ujumla, kuwa na joto la wastani na hivyo kutoathiri sana hali ya hewa nchini. Hata hivyo, ongezeko la joto linatarajiwa; hali hii ikijumuishwa na joto la juu ya wastani lililopo Kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi, inatarajiwa kusababisha mvua nyingi katika maeneo mengi ya nchi. Hali ya joto la wastani Kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantic (karibu na Angola) inatarajiwa kudhoofisha mvua katika maeneo ya Magharibi ya nchi pamoja na yale ya Ukanda wa Ziwa Viktoria.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA MWEZI FEBRUARI, 2017

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Mvua kadhaa, mara chache zikiambatana na ngurumo zinatarajiwa. Mvua hizi kwa ujumla zinatarajiwa kuwa za wastani.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): Mvua kadhaa, mara chache zikiambatana na ngurumo zinatarajiwa. Mvua hizi kwa ujumla zinatarajiwa kuwa za wastani.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): Mvua chache zitakazoambatana na ngurumo zinatarajiwa. Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Mvua kadhaa zitakazoambatana na ngurumo zinatarajiwa. Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Mvua kadhaa zitakazoambatana na ngurumo zinatarajiwa. Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani.

Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa na Mbeya): Mvua nyingi zitakazoambatana na ngurumo zinatarajiwa. Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Mvua nyingi zitakazoambatana na ngurumo zinatarajiwa. Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma): Mvua nyingi zitakazoambatana na ngurumo zinatarajiwa. Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani.

Imetolewa na; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**